BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Ishirini na Tisa – Tarehe 07 Juni, 2022
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. TAARIFA YA SPIKA:

## II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

### Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa mwaka 2022/2023.

### Mwenyekiti wa Kamati ya Uchumi:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Uchumi kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa Mwaka 2022/2023.

## III. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

144. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kuasisiwa kwa Kitambulisho cha Utambulisho wa Mzanzibari (ZanID) ni hatua moja ya kuuhuisha Uzanzibari. Hata hivyo, kumekuwa na sononeko la muda mrefu kutoka kwa wageni-wenyeji wenye asili ya Zanzibar ambao kwa sababu moja au

nyengine, wamekosa sifa ya kupatiwa Kitambulisho cha Utambulisho wa Mzanzibari (ZanID) lakini wana mchango mkubwa katika maendeleo ya Zanzibar ikiwemo kuipa sifa Zanzibar kimataifa kwa matendo yao duniani.

(a) Je, Serikali haioni haja ya kuwatambua Wazanzibari hao na kuwapatia Vitambulisho vya Wazanzibari Wasio Wakaazi (Non Resident Zanzibaris (NRZ)) sambamba na uraia mwengine walio nao.

(b) Je, ni upi msimamo wa Serikali kuhusu Utambulisho Pacha, kwa Wazanzibari Wasioishi Zanzibar na kwa Wageni Waishio Zanzibar.

(c) Je, hadi mwezi Machi 2022, watu wangapi wenyeji na wangapi wasio wenyeji wamesajiliwa na kupewa vitambulisho kama Wazanzibari Wakaazi au vitambulisho kama Wakaazi tu.

<u>**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**</u>

85. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kwa kuwa Serikali ilipitisha mishahara maalumu kwa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu za Ndani, na kwa kuwa asilimia kubwa ya Watendaji hao wamebahatika kupata mishahara hiyo mipya.

Je, ni upi mpango wa Serikali kwa Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu ambao wametimiza vigezo na wameshafanya kazi kwa muda mrefu bila ya kubadilishiwa mishahara yao na kupata haki yao hiyo.

<u>**Wizara ya Afya:**</u>

113. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kuna taarifa kwamba Hospitali ya Vitongoji (Vitongoji Cottage Hospital) kwa kipindi kirefu kumekuwa na tatizo la ubovu katika mfumo wake wa maji taka (Technical error in sewage system).

(a) Je, suala hili ni kweli.

(b) Kama ni kweli, Serikali imechukuwa hatua gani.

<u>**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**</u>

79. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa Skuli ya Msingi ya Wawi ni moja kati ya skuli kongwe sana hapa nchini, na kwa kuwa skuli hiyo imeendelea kuharibika siku hadi siku kutokana na uchakavu mkubwa wa majengo.

Je, ni upi mpango wa Serikali katika kuifanyia ukarabati skuli hiyo.

**<u>Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:</u>**

150. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

(a) Wizara ya Kilimo ina maofisa ugani wangapi kwa kila Wilaya na Je, kila mmoja anatoa huduma kwa wakulima wangapi.

(b) Je, idadi ya maofisa ugani inakidhi matakwa ya mahitaji ya wakulima wetu.

(c) Changamoto zipi zinawakabili maofisa ugani katika kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

**<u>Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:</u>**

98. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Miongoni mwa dhamira za Serikali ya Awamu ya Nane, ni kuwasaidia wajasiriamali mbali mbali.

Je, Serikali ina mpango gani wa kukisadia Kikundi cha Nguvu Hazichezewi kilichopo Mvumoni ambacho kinajishughulisha na ufugaji wa samaki na kilimo cha chumvi, ili wanakikundi hicho waweze kutekeleza shughuli zao kwa wepesi na kuweza kufaidika na kazi hiyo.

**Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:**

168. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Pamoja na jitihada za Serikali zote mbili na vyombo husika kujitahidi katika kuzuia idadi na ukubwa wa ajali za barabarani nchini, kumekuwa na idadi ya ajali za barabarani zinazosababishwa na matumizi ya simu kwa madereva wakiwa wanaendesha vyombo barabarani.

(a) Je, ni sheria ipi mahsusi inayokataza matumizi ya simu wakati dereva akiendesha gari.

(b) Je, ni ajali ngapi kwa mwaka 2021/2022 tayari zimesababishwa au zinadhaniwa kusababishwa na matumizi mabaya ya simu wakati wa kuendesha.

(c) Je, ni lini Serikali itatunga au kurekebisha sheria husika inayotekelezeka na yenye mwelekeo wa kupunguza ajali za barabarani zinazosababishwa na matumizi ya simu.

## IV. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Fedha na Mipango:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa mwaka 2022/2023.

Zanzibar,
07 Juni, 2022.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA